

University of Nairobi

# Ufundishaji wa Kiswahili Ulaya na Uchina: Modeli mbili na changamoto zao

Yuning Shen (Chuo Kikuu cha Ualimu cha Zhejiang)

[ynshen@outlook.com](mailto:ynshen@outlook.com)

2020/12/02 Webina ya “Kiswahili Ulimwenguni” Maadhimisho ya miaka 50 tangu kuasisishwa kwa Chuo Kikuu cha Nairobi

1 Modeli ya ufundishaji wa Ulaya

2 Modeli ya ufundishaji wa Uchina


3 Changamoto

4 Mapendekezo

# 1. Modeli ya ufundishaji wa Kiswahili Ulaya

## Dibaji

Ingawa fasihi ya Kiswahili ina historia ndefu, lakini taaluma—iliyoandikwa—ya fasihi ya Kiswahili haina umri mkubwa. Maandishi ya mwanzo kuhusu fasihi ya Kiswahili yalitolewa na Wazungu wa misioni kunako **karne ya kumi na tisa**. Waliokuwa mashuhuri katika uwanja huu ni **Ludwig Krapf** aliyekuwa na maskani yake Rabai, Mombasa na **Edward Steere**, aliyeshi Zanzibar. Krapf alikusanya miswada kadha ya tendi na kuipeleka Udachi mwanzo wa miaka ya 1840. Steere alishughulikia tendi, mashairi na hadithi simulizi. Kitabu chake maarufu zaidi cha fasihi ni *Swahili Tales* (London 1870). Baadaye walifuata Wazungu wengine kama **W. Taylor** *African Aphorisms* (London 1891), **Alice Werner** (miaka 1910–1930), **William Hichens** (miaka ya 1930-50). **Miaka hiyo ya 1880 hadi 1930** lilijitokeza pia kundi la wanataaluma wa Kidachi (**C. Velten, C. G. Buttner, K. Meinhof**, n. k.) ambalo lilitoa mchango mkubwa katika kukusanya, na kiasi kuchambua, fani za fasihi ya Kiswahili, hususan hadithi, nyimbo na mashairi. **Miaka ya 1940-60** Wazungu wengi zaidi walijitokeza kushughulikia uwanja huo; walio mashuhuri zaidi ni **Lyndon Harries, W. Whiteley, J. W. T. Allen, E. Dammann** na **H. E. Lambert**. Kipindi hicho vilevile ndipo wataalamu wenyeji



# 1. Modeli ya ufundishaji wa Kiswahili Ulaya

Bayreuth (Ujerumani): Universität Bayreuth

Berlin: Humboldt-Universität zu Berlin; Freie Universität Berlin (Chuo Kikuu Huria Berlin)

Edinburgh: The University of Edinburgh

Gothenburg (Sweden): Göteborgs universitet

Hamburg (Ujerumani): Universität Hamburg

Leiden (Uholanzi): Leiden University

London: SOAS University of London

Moscow: Московский государственный университет (Lomonosov Moscow State University)

Napoli (Italia): Università degli Studi di Napoli «L'Orientale»

Vienna (Austria): Universität Wien

Warsaw (Upolandi): Uniwersytet Warszawski

n.k. (k.m. Helsinki/Finland; Trondheim/Norway; Leipzig/Ujerumani; Cologne/Ujerumani)

# 1. Modeli ya ufundishaji wa Kiswahili Ulaya

	Modeli ya "African Studies"	
Mada kuu / Malengo	Maswala yote ya Afrika ikiwemo historia, tamaduni, siasa, uchumi, lugha	
Umuhimu wa lugha ya kiswahili kwenye mtaala	kozi ya kuchaguliwa kutoka lugha nyingine za kiafrika	
Muda wa masomo	Miaka miwili (mihula minne), kozi ya kuchaguliwa	
Wakati wa kuunga chuo kwa usajili	Kila mwaka wa masomo	
Lugha ya kufundishia	Kiingereza, pengine lugha rasmi ya chuo husika	

## 2 Modeli ya ufundishaji wa Kiswahili Uchina

■ Lugha ya Kiswahili kuwa mada ya kuu tangu mwaka wa 1960/1961

■ Vyuho vikuu muhimu zaidi kuanzia wakati huo mpaka sasa

- Beijing Foreign Studies University / Chuo Kikuu cha lugha za Kigeni, Beijing ->

- Communication University of China (Beijing) / Chuo Kikuu cha Mawasiliano ya Habari cha China ->

## 2 Modeli ya ufundishaji wa Kiswahili Uchina

	Modeli ya “African Studies”	Modeli ya BA ya Kiswahili (nchini Uchina)
Mada kuu / Malengo	Maswala yote ya Afrika ikiwemo historia, tamaduni, siasa, uchumi, lugha	Uwezo wa kutumia lugha ya Kiswahili (kusikiliza, kuongea, kusoma, kuandika), fasihi ya lugha ya kiswahili, taarifa ya Afrika Mashariki
Umuhimu wa lugha ya kiswahili kwenye mtaala	kozi ya kuchaguliwa kutoka lugha nyingine za kiafrika	Kama mada kuu na ya pekee
Muda wa masomo	Miaka miwili (mihula minne), kozi ya kuchaguliwa	Miaka minne, kozi ya lazima, muda wote
Wakati wa kuunga chuo kwa usajili	Kila mwaka wa masomo	kila baada ya miaka minne
Lugha ya kufundishia	Kiingereza, pengine lugha rasmi ya chuo husika	Mwanzo: Kichina Mwishoni: Kiswahili

# 2 Modeli ya ufundishaji wa Kiswahili Uchina

*SWAHILI FORUM 25 (2018): 158-164*

*SPECIAL ISSUE: Swahili Literature in Global Exchange: Translations, Translators and Trends, ed. by Uta Reuster-Jahn & Serena Talento*

## **HISTORIA FUPI YA TAFSIRI ZA VITABU VYA KISWAHILI NCHINI CHINA**

ZHAO LEI

---

Kuanzia mwaka 1964 hadi 1993, idara ya Kiswahili katika Shirika la Uchapishaji wa Lugha za Kigeni ilitafsiri na kuchapisha jumla ya vitabu 258 vya Kichina kwenda Kiswahili huku wasomi wa Kiswahili walitafsiri vitabu 26 vya Kiswahili kwa Kichina. Kwa kulinganisha idadi na maudhui ya vitabu hivyo katika enzi ya mapinduzi na ya mageuzi, makala hii inadhihirisha utegemezi wa tafsiri kwa sera ya serikali na mazingira ya jamii. Kwa hivyo, changamoto za kitaaluma na za kiuchumi zilizopo katika kutafsiri vitabu kwenda au kutoka Kiswahili nchini China zinakabili serikali, wachapishaji, waandishi, watafsiri na wasomaji kwa pamoja.



## 2 Modeli ya ufundishaji wa Kiswahili Uchina

Vyuo vingine vinavyoendeleza miradi ya BA ya lugha ya Kiswahili:

■ Tianjin Foreign Studies University (tangu 2007) ■ Shanghai International Studies University (tangu 2018)

Vyuo vinavyojaribu modeli inayofanana na "African Studies":

■ Peking University (Beijing) ■ Zhejiang Normal University (Jinghua/Yiwu, Zhejiang) ■ Vyuo vingine vichache



(Watumiaji wa Kamusi ya Kiswahili-Kichina, toleo kwenye mtandao, kuanzia mwaka w. 2013 hadi 2020)

# 2 Modeli ya ufundishaji wa Uchina



ias.zjnu.cn

## 浙江师范大学非洲研究院

Institute of African Studies Zhejiang Normal University

教育部省部共建协同创新中心  
外交部中非联合研究交流计划指导单位  
中非智库论坛创办单位、主办单位  
浙江省2011协同创新中心

教育部区域与国别研究重点培育基地  
外交部中非智库10+10合作计划中方智库  
浙江省新型重点专业智库

English • Français • Hausa • Kiswahili



ias.zjnu.cn/iaski/main.htm

## 浙江师范大学非洲研究院

Kitivo cha Utafiti wa Afrika cha Chuo Kikuu cha Ualimu cha Zhejiang

Habari fupi kuhusu | Wakuu wa Kitivo | Matawi ya Asasi | Maandalizi

Chinese




Kitivo cha Utafiti wa Afrika cha Chuo Kikuu cha Ualimu cha Zhejiang (IASZNU) ni kitivo cha kwanza cha utafiti wa kiumjamaa wa Afrika kilichoanzishwa na chuo kikuu nchini China. Kitivo hiki kiko mjini Jinhua, mkoa wa Zhejiang ulioko mashariki mwa China. Madhumuni ya kitivo hiki ni kujenga jukwaa la taaluma lililo wazi kwa upeo wa macho wa kimataifa wa kiwango cha juu, kukusanya watafiti


# 3. Changamoto za walimu na wanafunzi Ulaya na Uchina

- Ukosefu wa vitabu vinavyoandikwa kwa lugha ya kiswahili kwa ajili ya kufundisha historia, tamaduni na mambo mengine mbalimbali ya Afrika Mashariki
  - Mahitaji ya kuimarisha uhusiano wa ufundishaji wa lugha ya Kiswahili na ule wa lugha nyingine za kiafrika kwa uwiano wa (ma)taifa husika
  
- Ukosefu wa tuzo ya waandishi bora wa Kiswahili kwa Afrika Mashariki kwa ujumla
  
- Asilimia kubwa ya mikataba ya kazi ilifanyika baina ya chuo kikuu na walimu mmoja mmoja kibinafsi:
  - ukosefu wa ufadhili kutoka kwa taasisi ya taifa wala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;
  - Shida ya mawasiliano na ukosefu wa njia ya kujuliana hali kabla ya kutuma walimu

### 3. Changamoto za walimu na wanafunzi Ulaya na Uchina



Gabriel N. Chacha 1968. Historia ya [...]. Dar es Salaam: East African Literature Bureau.



Julius K. Nyerere 2016 (1994). Uongozi Wetu na [...] Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publisher.



# 4. Mapendekezo

- Kuhamasisha uandishi wa vitabu vinavyoeleza mambo ya Afrika Mashariki kwa lugha ya Kiswahili na uchapishaji wake
- Kuwashauri wachapishaji kwa kupitia sera maalum ili nao watoe nakala pacha kwa lugha ya Kiswahili ikiwa kama vitabu hivi havikuandikwa kwa lugha ya Kiswahili
- Kuunda taasisi maalum kwa kutathmini uwezo wa kutumia lugha ya Kiswahili (TOEFL/IELTS)



**Uhai wa Lugha ni matumizi yake! Ahsanteni!**

- MUWAKILISHAJI: Yuning Shen (Chuo Kikuu cha Ualimu cha Zhejiang)
- MADA: Ufundishaji wa Kiswahili Ulaya na Uchina: Modeli mbili na changamoto zao
- TAREHE: 2020/12/02 (Webina ya “Kiswahili Ulimwenguni“ Maadhimisho ya miaka 50 tangu kuasisishwa kwa Chuo Kikuu cha Nairobi)